

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA AROBAINI NA NNE

09 JUNI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA AROBAINI NA NNE – TAREHE 09 JUNI, 2023

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**567. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kwa nini Serikali haipeleki Fedha za Maendeleo kwa wakati katika Halmashauri nchini.

WIZARA YA KILIMO:

**568. MHESHIMIWA RAMADHANI ABEID
IGHONDO (SINGIDA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mkakati gani wa kufanya mageuzi ya Kilimo nchini.

WIZARA YA NISHATI:

569. MHESHIMIWA JAFARI WAMBURA CHEGE (RORYA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha umeme unafika kwenye Vitongoji vyote nchini.

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

570. MHESHIMIWA EMMANUEL LEKISHON SHANGAI (NGORONGORO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itapeleka mawasiliano katika Kata za Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

571. MHESHIMIWA DKT. FLORENCE GEORGE SAMIZI (MUHAMBWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itafanya ukarabati kwenye Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kibondo pamoja na nyumba za Askari Polisi.

**572. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMEDI
KUCHAUKA (LIWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itaunga mkono juhudi za ujenzi wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Liwale.

WIZARA YA MAJI:

**573. MHESHIMIWA ISSA JUMANNE MTEMVU
(KIBAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Wananchi wa Mpiji, Magohe, Kibesa, Msumi, Makabe, Msingwa, Ukombozi na Goba watapata maji safi na salama.

**574. MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI
(UKEREWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, upi mpango wa Serikali kumaliza kero ya upatikanaji wa maji safi na salama Wilayani Ukerewe.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

575. MHESHIMIWA HASAN SELEMAN MTENGA (MTWARA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, lini Serikali itawasaidia Wananchi wa Mtwara Mjini waliojiunga na *PRIDE* kurejeshewa fedha zao.

576. MHESHIMIWA DKT. FAUSTINE ENGELBERT NDUGULILE (KIGAMBONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, lini Mifumo ya Malipo ya Kimataifa itaruhusiwa ili Wabunifu/Watu wanaofanya kazi za ushauri kwa Taasisi za nje wapate malipo.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

577. MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU (ARUMERU MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Arusha – Mirongoine – Simanjiro – Terati hadi Kongwa kwa kiwango cha lami.

578. MHESHIMIWA TWAHA ALLY MPEMBENWE (KIBITI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Bungu hadi Nyamisati Wilayani Kibiti.

579. MHESHIMIWA FRANCIS KUMBA NDULANE (KILWA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini ujenzi wa njia nne kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Kilwa kipande cha Mbagala Rangi Tatu hadi Kongowe utakamilika.

**DODOMA
09 JUNI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**